**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Thelathini na Tatu – Tarehe 16 Juni, 2026**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

87. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Vikosi vya Idara Maalumu za SMZ vinafanyakazi nzuri katika majukumu yake mbalimbali ya kuimarisha amani na utulivu katika maeneo yetu. Hata hivyo, zipo baadhi ya operesheni za vikosi hivyo katika maeneo mbalimbali ya mji wetu hasa eneo la biashara Darajani, kudaiwa kufanya operesheni zake vikuhusisha matendo yanayokwenda kinyume na haki za binaadamu na utu wa watu, ikiwa ni pamoja na madai ya kutumia mbwa kudhibiti baadhi ya watu, huku akina mama ambao wakichaniwa nguo zao na wengine kung'atwa na mbwa hao.

(a) Pamoja na kazi nzuri ya vikosi vyetu, kwa nini Mamlaka zinaruhusu dosari kama hizo zijitokeze za kutumia mbwa kung'ata watu na kuchafua sifa nzuri ya vikosi vyetu.

(b) Je, kuna taratibu na kanuni gani zilizowekwa (rules of engagements) kwa vikosi vyetu pale vinaposhiriki operesheni mbalimbali, ili kuwe na mipaka katika kulinda haki za binaadamu bila ya kutweza utu wa mtu.

(c) Kwa dosari hizo zilizojitokeza, je kuna hatua zozote zimechukuliwa na Mamlaka husika kwa waathirika kupata haki zao na waliofanya kuchukuliwa hatua zinazostahiki.

189. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

Ofisi za masheha ni moja wapo ya matawi ya kiutawala ya Serikali Kuu yanayowaunganisha wananchi na Serikali moja kwa moja pamoja na kupata huduma za Serikali.

(a) Kwa nini wananchi wengi wanawalalamikia masheha katika shehia zao kwa kuwakosesha huduma muhimu kwa sababu zisizo za msingi.

(b) Je, ni vigezo gani ambavyo hutumika katika uteuzi wa masheha katika shehia za Zanzibar.

(c) Je, Serikali ipo tayari kushirikiana na wananchi katika Serikali za Mitaa ili kumpunguzia mamlaka ya kiutawala sheha.

<u>**Wizara ya Fedha na Mipango:**</u>

516. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa miaka mingi tumeona taasisi kadhaa hususani zinazokusanya mapato yasiyo ya kodi, zinashindwa kukusanya mapato kama zilivyokadiriwa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia ukomo wa bajeti (Budget ceiling) na kupelekea kuonekana hazifanyi vizuri lakini uhalisia ni kwamba walichokikusanya ndio uwezo walionao wa ukusanyaji.

Je, kuna miongozo gani inayotumiwa na Wizara yako katika kutoa ukomo wa bajeti kwa Wizara au taasisi za Serikali.

<u>**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**</u>

354. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wapo wananchi ndani ya jimbo la Ole ambao wamepitishiwa njia (line) kubwa ya umeme na wananchi hao wamezuiwa kujenga au kufanya shughuli yoyote ya kimaendeleo katika maeneo hayo.

Ni lini wananchi hawa watalipwa fidia ya maeneo yao ambayo yametumika kupitisha njia hiyo kubwa ya umeme.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

373. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Serikali inajenga nyumba za bei nafuu katika maeneo tofauti Unguja na Pemba.

(a) Ni upi mpango wa Serikali wa kuhakikisha kuwa inajenga nyumba za bei nafuu maeneo ya vijijini.

(b) Ni ipi tathmini ya Serikali katika kujenga nyumba za bei nafuu.

(c) Ni wazawa wangapi wamenunua nyumba hizo hadi sasa.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

528. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Kutokana na kuongezeka kwa watu na mahitaji ya viwanja, mahitaji ya viwanja vya kuchezea watoto yanaongezeka hasa wakati wa Skukuu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza msongamano katika viwanja vya kuchezea watoto katika Miji yetu.

**Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:**

50. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na kazi nzuri ya kuimarisha miundombinu ya barabara kuu na za ndani katika Mji wa Zanzibar, kwa lengo la kuimarisha huduma bora za usafiri salama kwa wananchi wake. Hata hivyo, kuna baadhi ya barabara hazijawekewa taa za barabarani na baadhi ya barabara zinazo taa za muda mrefu lakini hazifanyi kazi toka zilipowekwa.

(a) Je, kuna changamoto gani zinazosababisha taa hizo kutofanya kazi hasa katika barabara inayoanzia Fuoni Kibonde Mzungu mpaka kufikia Tunguu, ilhali taa hizo zimeshawekwa kwa muda mrefu.

(b) Kwa barabara ambazo hazina taa, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha barabara zote zinawekwa taa za barabarani.

(c) Je, kuna utaratibu maalumu wa kuzipitia taa za barabarani na kuzifanyia ukaguzi maalumu pamoja na matengenezo kwa kila kipindi, ili kuboresha utendaji kazi wa taa hizo.

411. MHESHIMIWA MARYAM SAID KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barabara ya Michungwani iliyopo katika jimbo la Ziwani imeshakuwa na ahadi nyingi sana za kujengwa huku hali yake ikiwa mbovu sana kiasi inapotokezea mgonjwa anabebwa kwa kitanda na hata kina mama wengi wanaotaka kujifungua, hupata shida sana kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Je, lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto :**

231. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, ni ipi mipango ya Serikali katika kuongeza Maafisa Ustawi wa Jamii katika Wilaya zote za Unguja na Pemba.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

206. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali ilitoa mpango ambao ungeliwezesha Ujenzi wa Chuo cha Amali katika eneo la Giningi, ndani ya jimbo la Chambani, ili kuwapunguzia usumbufu wanafunzi wa eneo hilo, pamoja na kuboresha huduma bora za upatikanaji wa elimu kwa wote.

(a) Ni lini Serikali itaanza kutekeleza mpango wa ujenzi wa mradi huo.

(b) Je, mchakato wa ujenzi wa mradi huo unatarajiwa kujumuishwa katika Mpango wa Serikali wa 2025-2030.

428. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kuna baadhi ya vyuo vimeanzisha masomo ya BOA kwa vijana wasiotimiza alama nzuri za kuendelea na Elimu ya Juu.

Je, utaratibu huu unatambulika kisheria.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

245. MHESHIMIWA ABDULGHANI ISMAIL ZUBEIR (Jimbo la Malindi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Serikali imekuwa na jitihada madhubuti ya kuziba pengo la kidijitali Serikalini na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa wananchi kupitia mifumo chini ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGaz).

(a) Je, ni mifumo mingapi mahususi ambayo eGaz imebuni na kuitengeneza wenyewe, tangu hatua ya usanifu mpaka utekelezaji, chini ya watalamu katika taasisi hiyo pekee.

(b) Je kuna taasisi au mifumo ya Serikali mingapi ambayo inajitegemea wenyewe na haisomani na mifumo mengine ya Serikali kama vile ZanMalipo.

(c) Ni hatua gani zimewekwa kuhakikisha watu wa vijijini na wenye kipato cha chini, wanaweza kupata huduma hizi za kidijitali.

473. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kwa sasa ulimwengu umejikita katika kuimarisha utendaji wake kwa kuitumia zaidi mifumo.

(a) Ni kwa kiasi gani Serikali inawapatia elimu watendaji wake, ili kwenda sambamba na mifumo tunayoitumia.

(b) Ni watendaji wangapi hadi sasa wamewezeshwa kupata taaluma hii.

**Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda:**

261. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwa muda mrefu wakulima wa karafuu wanalalamika kuhusiana na bei ya karafuu kuwa ndogo, kulingana na gharama za kuandaa mashamba.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa wakulima wa karafuu wanapata bei nzuri, ili wazidi kuhamasika na kuongeza uzalishaji wa karafuu.

(b) Serikali ina mikakati gani ya kuliongezea thamani zao la karafuu, badala ya kusafirisha karafuu ghafi, ili kuongeza mapato kwa Serikali na wananchi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

51. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Tunaipongea Serikali katika jitihada zake za kukusanya mapato kwa kutumia Mifumo ya Kielektroniki hasa mapato ya maegesho katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar. Hata hivyo, baadhi ya watendaji wa maeneo ya maegesho wanashindwa kusimamisha muda kwenye mfumo wakati gari zinapoondoka katika maegesho, kwa kutokuwepo eneo hilo au kufanya mambo mengine nje ya kazi zao. Hali hii inawaongezea wananchi bili kubwa ambayo haifanani na muda walioegesha magari yao kwa vile bado watakuwa wanahesabika kwenye mfumo kuwa wapo kwenye maegesho ilhali wameshaondoka muda mrefu.

(a) Kwa kiasi gani Serikali inaifahamu changamoto hiyo.

(b) Je, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha mifumo hiyo inakuwa fanisi katika kufanya kazi zake na kujiepusha zaidi kutegemea watu ambao wanaisababishia mifumo hiyo kutoa taarifa zisizo sahihi na kupelekea kuwahujumu wananchi.

224. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Chumbuni)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Wizara ilipanga kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Mahamamu Kijichi, Kizimbani, Forodhani na Hamamni pamoja na kuimarisha Mradi wa Eneo la Kihistoria Maruhubi Unguja.

Je, kuna sababu gani zilizopelekea maeneo hayo kutotekelezwa.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

131. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Je, Serikali ina mpango gani wa kifedha au sera za kiuchumi zitakazosaidia kuongeza ajira kwa vijana na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini.

385. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Ni jitihada zipi za Serikali za kutoa mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa wajasiriamali.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

142. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa uchumi wa buluu umetajwa kuwa chanzo kikubwa cha ajira Zanzibar.

Je, Wizara imeweka mikakati gani ya kuwapa vijana nafasi zaidi za ajira kupitia sekta ya uvuvi, ufugaji wa samaki na shughuli nyengine za baharini.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

177. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), kwa kipindi sasa imekuwa inapoteza imani kwa wananchi wa Zanzibar, hasa baada ya kukosa mwendelezo wa kesi ambazo hutokea na ambazo huzichunguza kutoka kwa viongozi, badala yake imekuwa kimya bila ya majibu yanayowatosheleza wananchi wa Zanzibar.

(a) Je, kwa sasa Mamlaka hii ina umuhimu na faida gani kwa wananchi wa Zanzibar.

(b) Ni sababu zipi zinazoipelekea Mamlaka hiyo kushindwa

kufuatilia upotevu wa mabilioni ya pesa za umma kila mwaka, ambayo hutolewa kwenye riport za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

(c) Ni kesi ngapi za upotevu wa pesa za umma kwa mwaka 2020 -2026 zilichunguzwa na ZAECA na kupelekwa Mahakamani.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**16 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR.**